

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA TANO

08 NOVEMBA, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA TANO – TAREHE 08 NOVEMBA, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

49. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ajira kwa Wahitimu wa Vyuo Vikuu hasa katika Sekta ya Kilimo kwa kuwa mikopo ya Elimu ya Juu imewezesha Wanafunzi wengi kuhitimu.

OFISI YA RAIS TAMISEMI:

50. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Zahanati katika Kata ya Ng'ambo iliyopo Tabora Mjini.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

51. MHESHIMIWA AMOUR KHAMIS MBAROUK (TUMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vikundi vya Wananchi ili kuhamasisha uhifadhi wa mazingira hasa katika Fukwe za Bahari ya Hindi.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

52. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:- Barabara ya Mlimani kutoka Mwembe – Mbaga hadi Mamba - Myamba ni kero kubwa kwa wakazi zaidi ya 150,000 katika Majimbo ya

Same Magharibi na Same Mashariki ambapo zaidi ya 70% ya wakazi wake wanaishi milimani:-

Je, ni lini barabara hiyo yenye urefu wa Km 120 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami nyepesi (*Surface dressing*) ili kufanikisha shughuli za maendeleo katika Wilaya ya Same.

53. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali imeweka vivutio gani maalum ili kuwavutia Wasafirishaji kutumia Bandari ya Mtwara kusafirisha mizigo ya nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

54. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-


Je, ni lini Serikali itaruhusu usafirishaji wa Viumbe Hai nje ya nchi.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

55. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la mawasiliano ya simu katika maeneo ya Bukiko, Chabilungo, Kitale na maeneo mengine yenye tatizo hilo Visiwani Ukerewe.



WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

56. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Vituo vya Polisi vilivyopo katika Kata za Kilema, Kirua Vunjo, Kahe na Marangu katika Jimbo la Vunjo vinapewa usafiri.

WIZARA YA KILIMO:

57. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itaondoa kabisa utaratibu wa kununua mazao kwa mkopo ambao unaendelea kutumiwa na baadhi ya Taasisi jambo ambalo linasababisha manung'uniko kwa Wakulima

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

58. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

- (a) Je, Serikali inayo *database* ya kutambua idadi ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi;
- (b) Je, nini mchango wa Watanzania wanaoishi nje ya Tanzania katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

III. KAMATI YA MIPANGO:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge lipokee, Kujadili na Kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka 2022/2023 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)



**DODOMA
08 NOVEMBA, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**